

Kitabu hiki kimejikita zaidi kueleza ukweli juu ya mapepo, maana zake, aina, majina, kazi na dawa yake. Ieleweke vema kwamba majini na mapepo ni maneno ambayo yamekuwa yakitumika kwa kupeana nafasi (interchangeable), hata hivyo dhana imeendelea kubakia moja japo majina hayo yamekuwa yakibadilika kutokana na imani kwa mfano wakristo walio wengi wanatumia zaidi neno mapepo wakati imani nyingine wamekuwa wakitumia neno majini. Viumbe hawa ni roho zisizoonekana kwa macho ya mwili japo hufanya kazi ama kuvaa umbo la kiumbe aonekanaye kwa macho kama vile binadamu, paka, ng'ombe n.k au kumtumia kiumbe halisi mfano kukaa ndani ya mtu anayefahamika au mnyama. Roho hizi zimeendelea kuwatesa watu kwa lengo moja kubwa ili wafarakane na Mungu wao hatimaye kuiacha imani yao nzuri na halisi ya Kristo. Hivyo basi kitabu hiki kitakuwa msaada mkubwa kwa watu walio ndani ya kanisa na nje ya kanisa kwani kitawawezesha kubaini siri ya mapepo na hatimaye kupata namna na uwezo wa kuyashinda, hatimaye kuwa na maisha ya furaha yasiyo na mateso. Ndiyo lengo hasa la mwandishi kwani amepata uzoefu wa kutosha juu ya mapepo na kwa mamlaka aliyopewa na Mungu mwenyewe ameona ni vema aweke wazi siri ya mapepo kwani kuna watu wengi wanaoonekana na mapepo katika maisha yao. Unaweza kuona uvivu kusoma kitabu hiki ama usikielewe lakini na kuisisitiza usome mpaka mwisho maana shetani hapendi ufunguliwe.

Kumbuka imeandikwa:- “Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya mapepo wabaya katika ulimwengu wa roho” Efeso 6:12 Binadamu tumepewa mamlaka kubwa juu ya viumbe wote lakini inahitajika imani thabiti katika Yesu Kristo na elimu juu ya viumbe hawa wabaya.

Karibu

Mwl. Peter Kajolo kapagi